



DOERNBECHER
CHILDREN'S
Hospital

Je, kiti chako cha gari ni bandia au ambacho hakijaidhinishwa?

Yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia unaponunua au kutumia kiti cha gari ili kumsafirisha mtoto wako. Je, kiti chako cha gari kinatimiza viwango vya usalama vya Marekani? Viti vya magari vilivyotengenezwa kwa ajili ya nchi zingine havitimizi viwango vyote vya usalama vinavyohitajika vya Marekani na viti bandia vya magari si salama kwa matumizi.

Kilichoidhinishwa



Onyo la mfuko wa hewa na hatari ya kukosa hewa linaloamrisha na shirikisho



Kiti kina kishikizo cha kifua na mshikizo wenye sehemu tano ulio na kanda za nyonga



Maelezo mengi katika upande wa kiti, ikiwa ni pamoja na vikomo vya uzani na kimo, maandishi ya shirikisho kuhusu matumizi kwenye magari, kibandiko cha ziada cha maelezo ya mawasiliano ya mtengenezaji, tarehe ambayo kiti kilitengenezwa, na nambari ya toleo

Ambacho hakijaidhinishwa au ni bandia



Lebo ya kawaida ya onyo iliyo na maelezo



Hakuna kishikizo cha kifua na hakuna kanda za nyonga




Maelezo machache, vibandiko vinaweza kuwepo au kutokuwepo, hakuna maelezo ya mtengenezaji au toleo

Kilichoidhinishwa

Ambacho hakijaidhinishwa au ni bandia




Lebo katika kitako cha kiti cha gari



Hakuna lebo



Kamba za chini za kufunga zinazohitajika na shirikisho




Hakuna kamba za chini za kufunga, wenzo hafifu ya kuachilia kitako, kitako kinaweza kutokuwepo

Viashirio vingine



Kishikizo cha kitambaa kinachohitajika na shirikisho katika kiti cha gari



Lebo inayohitajika na shirikisho inasema: Mfumo huu wa kufunga mtoto unatimiza viwango vyote vya usalama vinavyohusika vya magari vya Shirikisho.



Kadi inayohitajika na shirikisho ya kurejesha bidhaa itajumuishwa pamoja na kiti cha gari. Hii itakuwa na maelezo ya mtengenezaji na iko tayari kutumwa kwa barua.

Hatua zinazofuata

Ikiwa unahisi kwamba huenda una kiti cha gari ambacho hakijaidhinishwa/ni bandia, tafadhali fuata hatua hizi zinazofuata ili kuhakikisha usalama wa mtoto wako.

- ACHA kutumia kiti chako cha gari, omba kimoja kutoka kwa rafiki au ununue kipya mwenyewe (Walmart, Target, nk.)
- Wasiliana na Doernbecher Injury Prevention Program (Mpango wa Kuzuia Majeraha wa Doernbecher) kwa 503-418-5666 au utume barua pepe kwa safety@ohsu.edu na Fundisanifu Aliyeidhinishwa wa Viti vya Magari atashirikiana nawe ili kuhakikisha kwamba mtoto wako anasafiri kwa usalama
- Pia unaweza kupata Fundisanifu Aliyeidhinishwa wa Usalama wa Abiria Mtoto katika SafeKids.org